ISSN 0856 - 034X

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

***Supplement No. 38*** ***6th October, 2023***

***SUBSIDIARY LEGISLATION***

*To The Gazette of the United Republic of Tanzania No. 39 Vol. 104 Dated 6th October, 2023*
Printed by The Government Printer, Dodoma by Order of Government

TANGAZO LA SERIKALI. 716 la tarehe 6/10/2023

SHERIA YA USIMAMIZI WA MAZINGIRA
(SURA YA 191)

# KANUNI

*(Zimetengezwa chini ya kanuni ya 230(2)(s))*

KANUNI ZA MAREKEBISHO YA KANUNI ZA UTHIBITI NA USIMAMIZI WA BIASHARA YA KABONI ZA MWAKA 2023

Jina la Kanuni

TS. Na. 637 ya 2022

1. Kanuni hizi zitajulikana kama Kanuni za Marekebisho ya Kanuni za Udhibiti na Usimamizi wa Biashara ya Kaboni za mwaka 2023 na zitasomwa pamoja na Kanuni za Udhibiti na Usimamizi wa Biashara ya Kaboni za mwaka 2022 ambazo katika marekebisho haya zitarejewa kama "Kanuni Kuu".

Marekebisho ya Jina la Kanuni

2. Kanuni kuu zinarekebishwa katika jina la Kanuni kwa kuongeza maneno "Mifumo ya" mara baada ya neno "Biashara ya".

Marekebisho ya kanuni ya 2

3. Kanuni kuu zinarekebishwa katika Kanuni ya 2 kwa kufuta neno "mradi" linalojitokeza katika kanuni ya 2 na badala yake kuandika neno "mifumo".

Marekebisho ya kanuni ya 3

4. Kanuni kuu zinarekebishwa katika kanuni ya 3 kwa-

(a) kufuta maneno "kwa ajili ya kuuzwa kwenye biashara ya kaboni" yanayojitokeza mwisho wa

tafsiri ya neno “viwango vya Kaboni” na badala yake kuandika maneno “au kuondolewa kilichothibitishwa kwa kuzingatia Viwango vya Kimataifa vya Biashara ya Kaboni ambavyo vinarejewa kama viwango vya upunguzaji wa kaboni vilivyothibitishwa au kuidhinishwa”;

(b) kuongeza-

(i) katika tafsiri ya neno “biashara ya kaboni” maneno “au kuhamisha” mara baada ya neno “kununua”;

(ii) tafsiri za maneno mapya katika mtiririko wa kialfabeti unaotakiwa kama ifuatavyo-

““Kamati” maana yake ni Kamati kitaifa ya kitaalamu ya kutathimini miradi ya kaboni iliyoanzishwa chini ya kanuni ya 11(1);

“Mkataba” maana yake ni Mfumo wa Mkataba wa Umoja wa Kimataifa juu ya Mabadiliko ya Tabianchi;

“Mapato Ghafi” maana yake ni mapato yote yanayotokana na mauzo ya viwango vya kaboni kabla ya kuondoa gharama zozote au hasara;

“Mifumo” maana yake mtazamo wa sokoni au usio wa sokoni unaolenga kutekeleza shughuli za tabia nchi ambao unaruhusu matarajio makubwa katika kupunguza na kurekebisha, kuhamasisha maendeleo endelevu na msimamo wa kimazingira kama unavyotambulika katika mkataba wa kimataifa, itifaki ya Kyoto na makubaliano ya Paris;

"Mali" maana yake ni kitu kinachomilikiwa na mtu kinachotumika kwa lengo la uzalishaji wa viwango vya kaboni katika biashara ya kaboni;

"Miradi ya REDD+" maana yake ni miradi ya kupunguza uzalishaji wa hewa ya kaboni kutokana na upotevu na uharibifu wa misitu;

"Masjala ya Taifa ya Kaboni" maana yake ni ofisi inayotunza taarifa, takwimu na kumbukumbu mbalimbali zinazohusu masuala ya viwango vya kaboni vinavyokubalika kitaifa na kimataifa, iliyoanzishwa kwa mujibu wa Kanuni ya 38 (1);

"Msajili" maana yake ni mtu anayewajibika kutunza na kudumisha Masjala ya Taifa ya Kaboni; na

"mauzo" maana yake ni ubadilishanaji au uhamishaji wa viwango vya kaboni au fedha."

Marekebisho ya kanuni ya 5

5. Kanuni kuu zinarekebishwa katika kanuni ya 5 kwa kufuta-

(a) katika kanuni ndogo ya (1) neno-

(i) "ni" linalojitokeza baina ya neno "hizi" na "kuweka" na badala yake kuandika maneno "litakuwa ni"; na

(ii) "miradi ya" linalojitokeza baina ya neno "wa" na "biashara" na badala yake kuandika neno "mifumo";

(b) kanuni ndogo ya (2) na kuiandika upya kama

ifuatavyo-"

"(2) Katika kuhamasisha kutimiza lengo lililorejewa katika kanuni ndogo ya (1), kanuni hizi-

(a) zitaweka mfumo wa kisheria unaotakiwa kuhakikisha utunzaji endelevu wa mazingira na kutoa mchango wa nchi katika jitihada za kimataifa katika kupunguza uzalishaji wa gesijoto;

(b) zitahasisha upatikaji wa fedha kutoka vyanzo vya ndani na nje zitakazosaidia katika shughuli za kupunguza uzalishaji wa gesi joto na kuchochea uwekezaji endelevu."

(c) zitawezesha kujenga uwezo kwa ajili ya kukabiliana na kuhimili mabadiliko ya tabianchi."

Marekebisho ya kanuni ya 6

6. Kanuni kuu zinarekebishwa katika kanuni ya 6 kwa-

(a) kuongeza katika kanuni ndogo ya (1), neno "mifumo ya" kabla ya neno "biashara";

(b) kufuta kanuni ndogo ya (3) na kuiandika upya kama ifuatavyo-

"(3) Kwa kuzingatia kanuni ndogo ya (1) na (2), Waziri atakuwa na mamlaka ya kutoa barua ya kuidhinisha kwa ajili ya kutekeleza mfumo wa biashara ya kaboni ambao unakidhi vigezo muhimu vinavyohitajika."

Marekebisho ya kanuni ya 9

7. Kanuni kuu zinarekebishwa katika kanuni ya 9-

(a) katika kanuni ndogo ya (1)-

(i) kwa kufuta aya (e);

(ii) kuongeza aya mpya ya (n) mara baada ya aya ya (m) kama ifuatavyo:

"(n) kuratibu na kutekeleza shughuli

za kukuza uelewa wa umma kuhusu mifumo ya biashara ya kaboni;"

(iii) kuzipanga upya aya ya (f) mpaka (n) kama aya ya (e) mpaka aya (m) kama inavyotakiwa; na

(b) kuongeza kanuni ndogo ya (3) mara baada ya kanuni ndogo ya (2) kama ifuatavyo:

"(3) Bila kuathiri masharti ya kanuni hii, Mamlaka ya Taifa ya Uratibu au Mratibu wa Kitaifa itaanzisha Masijala ya Taifa ya Kaboni."

Marekebisho ya kanuni ya 11

8. Kanuni kuu zinarekebishwa kwa kufuta kanuni ya 11 na kuiandika upya kama ifuatavyo:

"Kamati ya Taifa ya Kutathmini Mifumo ya Biashara ya Kaboni

11.-(1) Wizara yenye dhamana na Mazingira itaanzisha Kamati ya Taifa ya Kutathmini ya Mifumo ya Biashara ya Kaboni.

(2) Kamati ya Taifa ya Kutathmini Mifumo ya Biashara ya Kaboni itakuwa na wajumbe kama ilivyoainishwa katika Jedwali la Kwanza.

(3) Kamati itakuwa chombo cha ushauri kwa Mamlaka ya Taifa au Mratibu wa Kitaifa.

(4) Bila kuathiri masharti ya kanuni ndogo (1) na (2), wajumbe wa Kamati watatumikia kwa muda wa miaka mitatu na wanaweza kuteuliwa tena kwa kipindi kingine kimoja.

(5) Kamati inaweza kumualika mtu yeyote kwa ajili ya kutoa utaalam kwa kadri itakavyohitajika.

(6) Mkurugenzi atakuwa mwenyekiti wa Kamati.

(7) Kamati ya Kitaifa ya

Kutathmini Mifumo ya Biashara ya Kaboni itaamua taratibu za uendeshaji wa shughuli zake."

Marekebisho ya kanuni ya 14

9. Kanuni kuu zinarekebishwa katika kanuni ya 14 kwa-

(a) kufuta neno "na" linaloonekana mwishoni mwa aya ya "(b)"; na

(b) kuongeza aya mpya mara baada ya aya ya (c) kama ifuatavyo:

"(d) kutambua na kuainisha maeneo mahsusi kwaajili ya mifumo ya biashara ya kaboni; na

(e) kufuatilia na kutathimini mifumo ya biashara ya kaboni na kuwasilisha taarifa kwa Mamlaka ya Taifa ya Uratibu au Mratibu wa Kitaifa"

Marekebisho ya kanuni ya 15

10. Kanuni kuu zinarekebishwa katika kanuni ya 15 kwa kuongeza maneno "Tawala za Mikoa na" katikati ya neno "ya" na "serikali".

Marekebisho ya kanuni ya 17

11. Kanuni kuu zinarekebishwa katika kanuni ya 17 kwa-

(a) kuongeza maneno "ndani ya maeneo yao ya utawala" mara baada ya neno "yafuatayo"; na

(b) kufuta-

(i) aya ya (a) na kuiandika upya kama ifuatavyo-

"(a) kusimamia miradi ya biashara ya kaboni kwa kushauriana na sekretarieti ya mkoa;"

(ii) katika aya ya (c), (e), (f) na (i) maneno "katika maeneo yao ya utawala"

(iii) katika aya ya (b) maneno "katika ngazi ya halmashauri".

Marekebisho ya kanuni ya

12. Kanuni kuu zinarekebishwa katika kanuni ya 18 kwa-

18

(a) kubadilisha maudhui ya kanuni ya 18 kuwa kanuni ndogo ya (1); na

(b) kuongeza kanuni ndogo ya (2) mpya mara baada ya kanuni ndogo ya (1) kama ifuatavyo:

"(2) Bila kuathiri masharti ya aya ya (c) mmiliki wa mradi anaweza kuingia katika makubaliano ya maafikiano au utaratibu unaofaa kwa madhumuni ya kulinda nia ya kujihusisha na mradi wa biashara ya kaboni."

Marekebisho ya kanuni ya 19

13. Kanuni kuu zinarekebishwa katika kanuni ya 19 kwa kufuta nambari "41" inayojitpkeza katika aya ya (g) na badala yake kuandika nambari "42".

Marekebisho ya kanuni ya 24

14. Kanuni kuu zinarekebishwa katika kanuni ya 24-

(a) katika kanuni ndogo ya (1) kwa-

(i) kuongeza aya mpya ya (g) mara baada ya aya ya (f) kama ifuatavyo-

"(g) maelezo juu ya mgawanyo wa faida kwa asilimia;"

(ii) kuzipanga upya aya ya (g), (h), (i), (j), na (k) kama aya (h), (i), (j),(k) na (l);

(b) kwa kuongeza kanuni ndogo mpya mara baada ya kanuni ndogo ya (2) kama ifuatavyo-

"(3) Endapo mpendekezaji wa mradi ataonesha nia ya kutumia viwango vya kaboni vilivyozalishwa vyote au sehemu kuhesabika katika mchango wa taifa wa kukabiliana na mabadiliko wa tabianchi wa nchi au sehemu nyingine atatakiwa kuomba kibali cha kuhamisha viwango hivyo kutoka kwa Mamlaka ya Taifa ya Uratibu au Mratibu wa Kitaifa kwa kuzingatia miongozo iliyoandaliwa kwa mujibu wa Ibara ya 6 ya Makubaliano ya Paris.

(4) Bila ya kuathiri kanuni ndogo ya (3), idhini itakuwa kwa mujibu wa methodolojia, utaratibu na viwango vilivyoainishwa vilivyokubalika na ya

kuhamisha viwango vilivyokubaliwa na mkutano mkuu wa nchi wanachama wa Makubaliano ya Paris.

(5) Bila kujali kanuni ndogo ya (3), Mamlaka ya Taifa ya Uratibu au Mratibu wa Kitaifa baada ya kuhakiki taarifa iliyopatiwa, itatoa barua ya idhini kupokea maombi kama ilivyoainishwa katika Jedwali la Pili.

(6) Bila kujali masharti ya kanuni ndogo ya (4) na (5), mtazamo wa mashirikino baina ya washiriki utakuwa kwa mujibu wa miongozo au mfumo uliyoandaliwa kwa mujibu wa ibara ya 6 ya Makubaliano ya Paris."

Marekebisho ya kanuni ya 26

15. Kanuni kuu zinarekebishwa katika kanuni ya 26 kwa kufuta-

(a) katika aya ya (a) neno "Kwanza" na badala yake kuandika neno "Tatu"; na

(b) katika aya ya (b) maneno "usajili wa" yanayojitokeza katikakati ya neno "ya" na "wa" na kuandika maneno "idhini ya";

(c) katika aya (c) maneno "usajili wa" yanayojitokeza katikati ya neno "kuhusu" na "wazo" na kuandika maneno "idhini ya";

(d) kufuta neno "atamuelekeza" yanayojitokeza katikati ya neno "kitaifa" na "mpendekezaji" na kuandika maneno "itatoa barua ya idhini kama ilivyoainishwa katika Jedwali la Nne kumuelekeza".

Marekebisho ya kanuni ya 27

16. Kanuni kuu zinarekebishwa katika kanuni ya 27 kwa-"

(a) Kufuta-

(i) katika kanuni ndogo ya (1) neno" kusajiliwa" linalojitokeza katikati ya neno "ya" na "kwa" na kuandika maneno "kupokea taarifa ya kuidhinishwa";

(ii) katika kanuni ndogo ya (3)(a) neno "Pili"

linalojitokeza katikati ya neno "jedwali" na ";" na kuandika neno "Tano";

(iii) katika kanuni ndogo ya (4)(a) neno "Tatu" linalojitokeza katikati ya neno "la" na ";" na kuandika neno "Sita"; na

(b) kuongeza-

(i) katika kanuni ndogo ya (2)-

(aa) katika aya ya (c) maneno "na jinsi mradi pendekezwa unavyoendana na sera, mipango na mikakati ya kitaifa" mara baada ya neno "mradi"

(bb) aya mpya mara baada ya aya (j) kama ifuatavyo-

"(k) mradi kuchangia katika mchango wa taifa uliopangwa."

(ii) katika kanuni ya (3)(b) maneno "au barua ya ridhaa" katikati ya maneno "mkutano" na "kwa";

Marekebisho ya kanuni ya 28

17. Kanuni kuu zinarekebishwa katika kanuni ya 28 kwa kufuta kanuni ndogo ya (9) na kuiandika upya kama ifuatavyo-

"(9) Mamlaka ya Taifa ya Uratibu au Mratibu wa Taifa baada ya kujiridhisha kwamba Andiko la mradi limekidhi vigezo vinavyohitajika itatoa barua ya uthibitisho ndani ya siku thelathini kutoka tarehe ya kupokea Andiko la mradi."

Marekebisho ya kanuni ya 29

18. Kanuni kuu zinarekebishwa katika kanuni ya 29 kwa kuongeza kanuni ndogo mpya mara baada ya kanuni ndogo ya (2) kama ifuatavyo-

"(3) Bila kuathiri kanuni ndogo ya (1) na (2), makubaliano ya ushirikiano katika miradi ya biashara ya kaboni yataingiwa kwa kuzingatia sheria na taratibu za nchi zinazoshiriki."

Marekebisho ya kanuni ya 34

19. Kanuni kuu zinarekebishwa katika kanuni ya 34-

(a) katika kanuni ndogo ya (3) kwa-

(i) kufuta-

(aa) maneno "matumizi ya ardhi" yanayojitokeza katikati ya maneno "yanayojihusisha" na ":" na kuandika maneno "miradi ya REDD+";

(bb) katika aya ya (a) maneno "yatokanayo na" na kuandika neno "ya"

(cc) katika aya ya (b)-

(aaa) neno "halmashauri" popote linapojitokeza na kuandika maneno "mamlaka za serikali za mitaa";

(bbb) neno kumi linalojitokeza katikati ya neno "asilimia" na "kati" na kuandika neno "nane";

(dd) katika aya ya (d)-

(aaa) maneno "mamlaka ya halmashauri" yanayojitokeza katikati ya maneno "ya" na "asilimia" na badala yake kuandika maneno" mamlaka za serikali za mitaa"; na

(bbb) neno "halmashauri" linalojitokeza katikati ya neno "kwa" na "kwa" na badala yake kuandika maneno "mamlaka za serikali za mitaa";

(ee) katika aya ya (e)-

(aaa) maneno "atalipa asilimia tisa" yanayojitokeza katikati ya neno "mpendekezaji" na "kwa" na kuandika maneno "atabakiza asilimia thelathini na moja na atalipa asilimia nane"; na

(bbb) neno "Pili" linalojitokeza katikati ya neno "la" na ";" na kuandika neno "Tano";

(ff) aya ya (f) na kuiandika upya kama ifuatavyo-

"(f) Mamlaka ya Taifa ya Uratibu au Mratibu wa Kitaifa italipa asilimia tatu kati ya asilimia nane kwenye mfuko wa Taifa wa Mazingir a kwa ajili ya kuwezesh a shughuli

za uhifadhi wa mazingira ikijumuisha nishati safi ya kupikia na teknolojia."

(ii) kuongeza aya mpya ya (c) mara baada ya aya ya (b) kama ifuatavyo-

"(c) kwa kuzingatia aya (b), asilimia mbili kati ya asilimia sitini na moja zitatolewa kwa Wizara yenye dhamana ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, ambapo asilimia moja itabaki kwa Wizara yenye dhamana na Tawala za Mikoa na Serikali za mitaa na asilimia moja itapelekwa kwa Sekretarieti ya Mkoa kuwezesha uratibu wa mifumo ya biashara ya kaboni na mipango mingine ya kuhifadhi mazingira"

(iii) kuzipanga upya aya ya (c), (d), (e) na (f) kama aya ya (d), (e), (f) na (g) kama inavyotakiwa.

(b) katika kanuni ndogo ya (4) kwa kuifuta na kuiandika upya kama ifuatavyo:

"(4) Bila kuathiri masharti ya kanuni ndogo ya (3)(a) na (e) kuhusu miradi isiyo ya REDD+ asilimia sitini na moja ambayo alipaswa kulipwa mmiliki na asilimia thelathini na moja ya mpendekezaji wa mradi, mgawanyo mpya unaweza kuamuliwa kwa majadiliano na mapatano kati ya mmiliki

na mpendekezaji wa mradi kuendana na aina ya mradi, wakati asilimia nane iliyobaki italipwa kwa Mamlaka ya Taifa ya Uratibu au Mratibu wa Kitaifa.";

Marekebisho ya kanuni ya 42

20. Kanuni kuu zinarekebishwa katika kanuni ya 42 kwa-

(a) kubadilisha maudhui ya kanuni ya 42 kuwa maudhui ya kanuni ndogo ya (1); na
(b) Kuongeza kanuni ndogo mpya ya (2) mara baada ya kanuni ndogo ya (1) kama kama ifuatavyo:

"(2) Bila kuathiri kanuni ndogo (1), utaratibu wa kufuatilia na kutathmini miradi inayosaidia kufikiwa kwa malengo ya mchango wa taifa wa kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi itafanyika kwa kuzingatia mfumo wa upimaji, uwasilishwaji na uhakiki wa mchango huo."

Marekebisho ya kanuni ya 48

21. Kanuni kuu zinarekebishwa katika kanuni ya 48 kwa kuongeza kanuni ndogo mpya ya (4) mara baada ya kanuni ndogo ya (3) kama ifuatavyo:

"(4) Bila kuathiri masharti ya kanuni ndogo ya (1), (2) na (3), miradi inayotekelezwa chini ya utaratibu wa mfumo wa miradi ya maendeleo safi kwa mujibu wa Ibara ya 12 ya Itifaki ya Kyoto italazimika kuhama kwenda kwenye mifumo inayotekelezwa chini ya Ibara ya 6.4 ya Makubaliano ya Paris kwa kuzingatia taratibu zilizokubaliwa na mkutano wa nchi wanachama wa Itifaki ya Kyoto."

Marekebisho ya Jedwali la Kwanza

22. Kanuni kuu zinarekebishwa kwa kufuta Jedwali la Kwanza na kuliandika upya kama ifuatavyo:

"___________

JEDWALI LA KWANZA

___________

*(Limetengenezwa chini ya kanuni ya 11(2))*

MUUNDO WA KAMATI YA KIUFUNDI YA KITAIFA YA KUTATHMINI MIRADI YA KABONI

1. Kamati ya Wataalamu ya Kitaifa ya Kutathmini Miradi ya Kaboni itajumuisha wajumbe wafuatao:
   (a) Mkurugenzi wa Mazingira ambaye atakuwa Mwenyekiti wa Kamati;
   (b) Msajili ambaye atakuwa Katibu wa Kamati;
   (c) Mkurugenzi wa Idara ya Huduma za Sheria wa Wizara yenye dhamana ya masuala ya Mazingira;
   (d) Kamishina wa Fedha za Nje kutoka Wizara yenye dhamana ya masuala ya Fedha;
   (e) Mkurugenzi wa Idara ya Ushirikiano wa Kimataifa kutoka kwa Wizara yenye dhamana ya masuala ya Mambo ya Nje;
   (f) Wajumbe wengine kumi (10) ambao watatoka kwenye wizara, idara, wakala na taasisi za Serikali, asasi za kiraia, taasisi za elimu na sekta binafsi wenye sifa au uzoefu wa masuala ya mabadiliko ya tabianchi, mazingira, usimamizi wa maliasili, ushirikiano wa kimataifa, biashara ya kaboni na taaluma yoyote inayohusiana na masuala haya.

| | |
|---|---|
| Marekebisho ya Jedwali la Pili | 23. Kanuni kuu zinarekebishwa kwa kufuta Jedwali la Pili na kuliandika upya kama ifuatavyo: |

"___________

JEDWALI LA PILI

__________

*(Limetengenezwa chini ya kanuni ya 24(5))*

BARUA YA IDHINI YA KUHAMISHA VIWANGO VYA KABONI

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA MAKAMU WA RAIS

Anwani ya simu: "MAKAMU",
Simu Na.: 2113857/2116995
Fax Na.: 2113856
Baruapepe: km@vpo.go.tz

Mji wa Serikali,
Eneo la Mtumba,
S.L.P 2502,
40406 Dodoma,
TANZANIA.

Unapojibu taja

Kumb: ……………………………………..
Tarehe:……………………

Anuani ya Mwombaji:

YAH: IDHINI YA ____________ (TAJA JINA LA MRADI)

Rejea somo tajwa hapo juu.

2. Jamhuri ya Muungano ya Tanzania ni nchi mwanachama wa Mikataba ya Umoja wa Mataifa kuhusu Mabadiliko ya Tabianchi (UNFCCC), Itifaki ya Kyoto na Makubaliano ya Paris.

3 Ofisi ya Makamu wa Rais kama Mamlaka ya Taifa ya Uratibu na Mratibu wa Kitaifa inadhamana ya kusimamia ushiriki wa Tanzania katika utekelezaji wa miradi ya ushirikiano kwa mujibu wa ibara ya 6.2 ya Makubaliano ya Paris na uamuzi namba 2/CMA3 chini ya makubaliano haya.

4. Ofisi ya Makamu wa Rais baada ya kupitia mapendekezo ya Kamati ya Wataalamu ya Kitaifa ya Kutathmini Miradi ya Kaboni kuhusu maombi ya idhini ya kuhamisha kiasi cha kaboni kutoka_________________ (Taja jina la mradi) imeidhinisha kuhamishwa kwa kiasi cha ______________ (Taja kiasi) kilichozalishwa wakati wa utekelezwaji wa Mradi wa Ushirikiano kati ya _________________ (Taja majina ya washirika) kwa mujibu wa ibara ya 6.2 ya Makubaliano ya Paris kwa kipindi kuanzia________________ hadi_____________

5. Tunakushukuru kwa ushirikiano wako.

Lakiri ya Ofisi

……………………..
WAZIRI MWENYE DHAMANA YA MAZINGIRA"

| | |
|---|---|
| Marekebisho ya Jedwali la Tatu | 24. Kanuni kuu zinarekebishwa kwa kufuta Jedwali la Tatu na kuliandika upya kama ifuatavyo: |

"

JEDWALI LA TATU

*(Limetengenezwa chini ya kanuni ya 26(a))*

FOMU YA MAOMBI YA BIASHARA YA KABONI

Jina la mradi unaopendekezwa: ……………………………..……………...……………………
Namba ya kumbukumbu ya maombi ya mradi: ……………………………………………..
Tarehe ya maombi: ……………………………………………………..……….……………
Aina ya mfumo au mbinu zinazopendekezwa kutumika
………………………………………………………………………………………
Maelezo ya kina ya mradi

A. Maelezo ya mradi, aina, eneo, ukubwa na ratiba ya utekelezaji

| | Maelezo ya jumla | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| A.1 Maelezo ya mradi kwa ufupi na shughuli zinazopendekezwa (Mradi unahusu shughuli gani, malengo, manufaa yanayotarajiwa, muda wa utekelezaji, bajeti na uhusiano wa mradi na vipaumbele vya Taifa n.k (Maneno yasizidi 250) | | | | | |
| A.2 Je, Mpendekezaji wa mradi ni Mmiliki? | NDIYO | | HAPANA | | Maoni |
| Kama ni hapana: | Ambatisha idhini kutoka kwa Mmiliki | | | | |
| | | | | | |
| Mpendekezaji wa mradi anayesajili Andiko la Awali la Mradi | | | | | |
| A.3 Jina la Mpendekezaji wa Mradi | | | | | |
| A.4 Aina ya taasisi (chagua moja au zaidi) | (a) Wizara, Idara au Wakala<br>(b) Serikali za Mitaa (Halmashauri ya Jiji, Halmashauri ya Manispaa, Halmashauri ya Wilaya, Halmashauri ya Mji, Mtaa au Serikali ya Kijiji)<br>(c) Kampuni au mtu binafsi<br>(d) Asasi za kiraia | | | | |
| A.5 Kazi nyingine za Mpendekezaji wa mradi (chagua moja au | (a) Mfadhili<br>(b) Dalali<br>(c) Mshauri wa kitaalamu | | | | |

| | |
|---|---|
| zaidi) | |
| A.6 Maelezo kuhusu uzoefu | |
| A.7 Anwani | |
| A.8 Mhusika wa kupokea mawasiliano | |
| A.9 Simu / nukushi | |
| A.10 Baruapepe na tovuti | |
| Mmiliki | |
| A.11 Jina la Mmiliki | |
| A.12 Aina ya taasisi (chagua moja au zaidi) | (a) Wizara, Idara au Wakala<br>(b) Serikali za Mitaa (Halmashauri ya Jiji, Halmashauri ya Manispaa, Halmashauri ya Wilaya, Halmashauri ya Mji, Mtaa au Halmashauri ya Kijiji)<br>(c) Kampuni au mtu binafsi<br>(d) Asasi za kiraia |
| A.13 Anwani | |
| A.14 Mhusika wa kupokea mawasiliano | |
| A.15 Simu / nukushi | |
| A.16 Baruapepe na tovuti | |
| Mfadhili wa mradi au mnunuzi wa Viwango vya kaboni<br>(Orodhesha na toa maelezo kuhusu wafadhili wote wa mradi) | |
| A.17 Jina la Mfadhili | |
| A.18 Aina ya taasisi (chagua moja au zaidi) | (a) Serikali<br>(b) Wakala wa Serikali<br>(c) Jiji au Manispaa n.k<br>(d) Kampuni au mtu binafsi<br>(e) Asasi za kiraia |
| A.19 Anwani (Jumuisha anwani ya tovuti) | |
| A.20 Shughuli kuu za mradi | |
| A.21 Maelezo kuhusu mali na fedha (jumla ya mali, mapato, n.k.) | |
| Aina ya Mradi | |
| A.22 Aina ya gesijoto zinazolengwa | |
| A.23 Aina ya shughuli | (mf: ufyonzaji/uhifadhi) |
| Eneo la Mradi | |
| A.24 Mkoa | |

| | | | |
|---|---|---|---|
| A.25 Wilaya | | | |
| A.26 Tarafa | | | |
| A.27 Kata | | | |
| A.28 Kijiji | | | |
| A.29 Eneo mahsusi la mradi (vibainishi vya GPS) | | | |
| Kama mradi wa kaboni unahusu msitu, elezea mfumo wa usimamizi wa msitu husika | | | |
| | NDIYO | HAPANA | Maoni |
| A.30 Je, kuna Mpango wa Usimamizi ulioidhinishwa? | | | |
| A.31 Je, kuna sheria ndogo zilizoidhinishwa? | | | |
| A.32 Je, kuna mgogoro wa ardhi au migogoro mingine? | | | |
| A.33 Je, msitu umependekezwa, umetamkwa au umetangazwa kwenye Gazeti la Serikali? | | | |
| A.34 Je, kuna Mpango wa Matumizi bora ya ardhi? (kama unahitajika) | | | |
| A.35 Je, mradi unahitaji kufanyiwa tathmini ya athari kwa mazingira? | | | |
| Ratiba ya utekelezaji | | | |
| A.36 Terehe ya kuanza mradi (mwaka ambao mradi utaanza kutekelezwa ikijumuisha muda wa kuanza mradi baada kupata idhini ya Andiko la Mradi) | | | |
| A.37 Mwaka unaotarajiwa kuanza kuuza viwango vya kaboni | mfano 2022/2023 | | |
| A.38 Muda wa kutekeleza mradi | | | |

| | |
|---|---|
| (Idadi ya miaka) | |
| A.39 Hali ya sasa na awamu za utekelezaji wa mradi | |

B. Faida za kimazingira na kijamii zinazotarajiwa

| Faida za kimazingira | |
|---|---|
| B.1 Makadirio ya kaboni itakayofyonzwa au kuhifadhiwa (katika tani za metriki za kabonidayoksaidi ambayo ni sawa – t CO2eq. Tafadhali ambatisha Jedwali.)<br>Weka makadirio na shughuli | mf. 2022: xx t CO2 eq<br>mf. 2023: xx t CO2 eq |
| B.2 Hali ya msingi<br>(Je, siku zijazo zingekuwaje bila mradi uliopendekezwa?<br>Makadirio ya ufyonzaji au uhifadhi wa kaboni kabla ya mradi uliopendekezwa yalikuwaje?<br>Taja mbinu utakazotumia kukokotoa hali ya msingi<br>Eleza namna mradi unavyozingatia matakwa ya miongozo.<br>Eleza kama shughuli za mradi haziwezi kufanyika pasipokuwepo kwa maradi, Taja vichocheo vikuu vya ukataji miti na jinsi mradi utakavyoshughulikia | |
| B.3 Uoto wa asili na matumizi ya ardhi<br>(Je, ni aina gani ya uoto wa asili uliopo na matumizi ya ardhi kwa sasa? Je, eneo la miti ni zaidi au chini ya asilimia kumi? Je, eneo hilo ni zaidi ya hekta 0.5?) | |
| B.4 Faida za kimazingira | |
| B.4.a Faida kwa jamii | |
| B.4.b Faida za kitaifa | |
| B.4.c Faida za kimataifa | |
| B.5 Ulinganifu kati ya mradi na vipaumbele vya mazingira nchini | |
| Faida za kijamii na kiuchumi | |
| B.6 Je, ni jinsi gani mradi utaboresha ustawi wa jamii inayohusika au inayozunguka mradi?<br>Je, ni athari gani za moja kwa moja ambazo zinaweza kuhusishwa na mradi na ambazo zisingetokea kama mradi usingekuwepo? (mf. ukusanyaji wa mapato, kutoa fursa za ajira, kupunguza umaskini, akiba ya fedha za kigeni). Ainisha idadi ya jamii na watu watakaonufaika na mradi huu. | |
| B.7 Je, kuna mpango wowote wa kuchangia mgawanyo wa gharama na faida? Kama jibu ni ndiyo weka kiambatisho | |
| B.8 Je, kuna faida nyingine? | |

| | |
|---|---|
| (mf. Mafunzo au elimu kutokana na kuanzishwa kwa teknolojia mpya na bidhaa, urudufishaji katika nchi, mkoa au wilaya) | |

C. Fedha

| Gharama za mradi | |
|---|---|
| C.1 Gharama za maandalizi ya mradi | Dola za Kimarekani |
| C.2 Gharama za uanzishwaji wa mradi | Dola za Kimarekani |
| C.3 Gharama zingine (elezea) | Dola za Kimarekani |
| C.4 Jumla ya gharama za mradi | Dola za Kimarekani |
| | |

Tamko

Mimi………………………………………………………. ninathibitisha kwamba, taarifa zilizotolewa katika maombi haya ni za kweli kadiri ya uelewa wangu.

Muhuri wa Ofisi

Jina:………………………………..
Wadhifa:……………………........
Saini:……………………………
Tarehe:………………………………….

Imeshuhudiwa na-
Jina:………………………………..
Wadhifa:……………………........
Saini:……………………………
Tarehe:………………………………….

Tafadhali ambatisha:
Katiba ya Kampuni (Memorandum and Articles of Association)
Cheti cha Usajili wa Biashara
Cheti cha Namba ya Utambulisho wa Mlipa Kodi
Leseni ya Biashara
Ritani ya Mwaka ya karibuni iliyosajiliwa BRELA ya Taarifa za Kampuni
Ripoti ya karibuni ya Taarifa ya Biashara/Kampuni kutoka BRELA"

| | |
|---|---|
| Marekebisho ya Jedwali la Nne | 25. Kanuni kuu zinarekebishwa kwa kufuta Jedwali la Nne na kuliandika upya kama ifuatavyo: |

« ______________

JEDWALI LA NNE
______________

*(Limetengenezwa chini ya kanuni ya 26(c) na (d))*

BARUA YA IDHINI YA KUANZISHA NA KUENDESHA MRADI WA BIASHARA YA KABONI

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA MAKAMU WA RAIS

Anwani ya simu:"MAKAMU",
Simu Na.: 2113857/2116995
Fax Na.: 2113856
Baruapepe: km@vpo.go.tz

Mji wa Serikali,
Eneo la Mtumba,
S.L.P 2502,
40406 Dodoma,
TANZANIA.

Unapojibu taja

Kumb: ……………………………………..
Tarehe:……………………

Anuani ya Muhusika:

YAH: IDHINI YA…………………….. [JINA LA MUHUSIKA WA BIASHARA YA KABONI ANAEOMBA IDHINI]

Tafadhali husika na somo tajwa hapo juu.

2. Serikali ya Tanzania imeidhinisha…………[jina la muhusika wa soko la mradi wa kaboni].

3. Serikali imeidhinisha…………..[Jina la muhusika wa soko la mradi wa Kaboni anaeomba barea ya idhini] kwa masharti yafuatayo:

(i) Shughuli za mfumo lazima ziorodheshwe na ziwe miongoni mwa malengo mkakati ya Mamlaka ya Taifa ya Uratibu iliyoidhinishwa au kuthibitishwa kusimamia Mradi…..……… [Jina la Kiambatisho].

(ii) Shughuli za mfumo lazima ziwe katika [masharti] au [zisizo na masharti] au [nje ya mawanda] ya kundi la maleango mkakati ya Mamlaka ya Taifa ya Uratibu.

(iii) Chombo cha Umma au Binafsi kinachoomba kuendeleza shughuli za mfumo lazima kiwe kimepokea barua ya idhini kutoka Mamlaka ya Taifa ya Uratibu juu ya namna ya kushiriki katika shughuli kama mshiriki katika mfumo.

(iv) Mamlaka ya Taifa ya Uratibu lazima itoe barua ya kusaidia maendeleo endelevu kuhusu mfumo kwa Chombo kilichoidhinishwa kushiriki katika shughuli hiyo kama mshiriki.

(v) Mshiriki wa Shughuli za Mfumo lazima atimize mitazamo ya msingi na matakwa ya kimethologia ikijumuisha kipindi cha nyongeza na cha kiwango kama kinavyotumika katika ibara ya 6.4 ya shughuli ambazo Tanzania inataka kusimamia katika mfumo.

(vi) Mshiriki wa shughuli za mfumo atawasilisha barua rasmi kwa Mamlaka ya Taifa ya Uratibu akiomba barua ya idhini.

(vii) Mshiriki wa mfumo alieidhinishwa lazima alipe ada kwa viwango vilivyoelezwa kwenye kanuni hii kwa ajili ya kupata barua ya idhini.

(viii) Mamlaka ya Taifa ya Uratibu itaitangaza kwa Umma barua ya idhini kwa kuihamishia kwa chombo kinachosimamia mfumo ndani ya muda saw ana ule wa kutoa barua ya idhini.

4. Asante kwa ushirikiano wako.

Lakiri ya Msajili

…………………………………………
MSAJILI
Kny: KATIBU MKUU"

| | |
|---|---|
| Marekebisho ya Jedwali la Tano | 26. Kanuni kuu zinarekebishwa kwa kufuta Jedwali la Tano na kuliandika upya kama ifuatavyo: |

"____________

JEDWALI LA TANO

____________

*(Limetengenezwa chini ya kanuni 26(b), 27(3)(a)) na 34(3)(e))*

ADA

| Na | Aina ya Ada | Kiasi | |
|---|---|---|---|
| 1. | Ada ya maombi | kwa raia | Dola za Kimarekani 250 ambazo zitalipwa kwa Shilingi za Tanzania |
| | | kwa asiye raia | Dola za Kimarekani 500 |
| 2. | Ada ya usajili | Asilimia 1 ya wastani unaotarajiwa wa mapato ya kila mwaka kutokana na mauzo ya kiasi cha Kaboni inayolipwa mara moja kwa maisha ya mradi kama itakavyoamuliwa na Mamlaka ya Taifa ya Uratibu au Mratibu wa Kitaifa kulingana na bei iliyopo ya soko la dunia. | |
| 3. | Ada ya uendeshaji wa mradi kwa mwaka | Asilimia 5 ya mapato ya jumla kutokana na mauzo ya mauzo ya kiasi cha Kaboni inayolipwa kila mwaka na Mpendekezaji | |
| 4. | Ada ya uendeshaji wa mradi kwa mwaka | Asilimia 3 ya mapato ya jumla kutokana na mauzo ya mauzo ya kiasi cha Kaboni inayolipwa kila mwaka na Mpendekezaji | |

| | |
|---|---|
| Kuongeza Majedwali | 27. Kanuni kuu zinarekebishwa kwa kuongeza majedwali mapya mara baada ya Jedwali la Tano kama ifuatavyo: |

"______________

JEDWALI LA SITA

______________

*(Limetengenezwa chini ya kanuni ya 27(4)(a))*

BARUA YA KUTOKUWA NA PINGAMIZI

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA MAKAMU WA RAIS

Anwani ya simu:"MAKAMU",
Simu Na.: 2113857/2116995
Fax Na.: 2113856
Baruapepe: km@vpo.go.tz

Mji wa Serikali,
Eneo la Mtumba,
P.O. Box 2502,
Dodoma,
TANZANIA.

Unapojibu taja

Kumb: ……………………………………..
Tarehe:……………………

Anwani ya Mpendekezaji…
………………………………..
………………………………..

YAH: Barua ya Kutokuwa na Pingamizi inayohusu mradi wa………………………………….
…………………………………………………………………………………………………

1. Rejea somo tajwa hapo juu na barua yako yenye kumbukumbu Na ………. …… …. ya tarehe …………….
2. Ofisi ya Makamu wa Rais imepokea na kupitia Andiko la Awali la Mradi unaopendekezwa.
3. Unataarifiwa kwamba -
   (a) Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni mwanachama wa (Futa isiyohusika) Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa Mabadiliko ya Tabianchi au Itifaki ya Kyoto au Makubaliano ya Paris.
   (b) Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania haina pingamizi na mradi uliopendekezwa kama ulivyowasilishwa kupitia Andiko la Awali la Mradi.
   (c) Mradi uliopendekezwa unaendana na sera, mikakati, mipango na vipaumbele vya nchi.
4. Ofisi inakujulisha kuwa, namba ya usajili wa mradi itawekwa hadharani kwa taarifa kwa umma kadiri inavyofaa.
5. Imesainiwa……………..………… na…………………………………..…………….

Muhuri

KATIBU MKUU

JEDWALI LA SABA

*(Limetengenezwa chini ya kanuni ya 28(10))*

BARUA YA IDHINI YA UTEKELEZAJI WA MRADI

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA MAKAMU WA RAIS

Anwani ya simu:“MAKAMU”,
Simu Na.: 2113857/2116995
Fax Na.: 2113856

Baruapepe: km@vpo.go.tz

Mji wa Serikali,
Eneo la Mtumba,
P.O. Box 2502,
Dodoma,
TANZANIA.

Unapojibu taja
Kumb: ……………………………………..
Tarehe:……………………

Anwani ya Mpendekezaji(w)…
………………………………..
………………………………..

YAH: Barua ya Uidhinishaji Mradi wa…………………………..……………………….

…………………………………………………………………………………………………

1. Rejea somo tajwa hapo juu na barua yako yenye kumbukumbu Na ………………. ya tarehe …………….
2. Ofisi ya Makamu wa Rais imepokea na kupitia Andiko la Awali la Mradi unaopendekezwa.
3. Unataarifiwa kwamba-
   (a) Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni mwanachama wa (Futa isiyohusika) Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa Mabadiliko ya Tabianchi au Itifaki ya Kyoto au Makubaliano ya Paris.
   (b) Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania haina pingamizi na mradi uliopendekezwa kama ulivyowasilishwa kupitia Andiko la Awali la Mradi.
   (c) Mradi uliopendekezwa unaendana na sera, mikakati, mipango na vipaumbele vya nchi.
4. Barua hii ni uthibitisho kwamba, mradi wako...................(Taja jina la mradi) umeidhinishwa, ambapo utatakiwa kuzingatia sheria za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na mikataba ya kimataifa inayosimamia biashara ya kaboni.
5. Ofisi inakujulisha kuwa, namba ya usajili wa mradi itawekwa hadharani kwa taarifa kwa umma kadiri inavyofaa.
6. Imesainiwa……………..…………..., ………………….…………….

Muhuri
KATIBU MKUU

JEDWALI LA NANE

*(Limetengenezwa chini ya kanuni ya 41(3))*

MUUNDO WA RIPOTI YA MWAKA

(Taarifa hii isizidi kurasa kumi)

Hali ya Utekelezaji wa Mradi

Jina la mradi: ……….………………..……………………………………………………………
Kipindi cha utekelezaji: ……….……………………………………………………………………
Imeandaliwa na: …………………………..……………………………………………………...

1. Ripoti ya utekelezaji wa mradi
   (a) Kazi zilizotekelezwa
      (i) Maelezo ya shughuli za mradi zilizotekelezwa katika kipindi cha kuripoti kulingana na mpango kazi;
      (ii) Viwango vya kaboni zilizozalishwa ikilinganishwa na viwango vya kaboni vilivyotarajiwa kuzalishwa kama ilivyoainishwa kwenye Andiko la Mradi; na
      (iii) Taarifa nyingine muhimu.

   (b) Taarifa za Fedha
   Taarifa ya fedha inayoonyesha muhtasari wa mapato yanayotokana na viwango vya kaboni vilivyouzwa na mgawanyo wa gharama na faida kwa wadau.

2. Matokeo ya mradi
   Tathmini fupi kuhusu kiwango ambacho malengo ya mradi yamefikiwa, ambayo itajumuisha-
   (a) Mafanikio katika ngazi ya jamii, taifa na kimataifa katika kujenga uwezo;
   (b) Utekelezaji wa Mchango wa Taifa wa Kukabiliana na Mabadiliko ya Tabianchi;
   (c) Kujenga uelewa;
   (d) uhaulishaji wa teknolojia;
   (e) Utunzaji wa Mazingira endelevu; na
   (f) Taarifa nyingine muhimu.

3. Hali Himilivu ya Usimamizi wa Mradi
   (a) Changamoto na fursa (Maelezo ya hali iliyosabibisha kubadilika kwa utekelezaji wa shughuli za mradi ikilinganishwa na mpango kazi wa mradi);
   (b) Tathmini ya vihatarishi na fursa zinazotarajiwa (tathmini ya vihatarishi vya ndani au nje ya Mradi) ambavyo vinaweza kuathiri mafanikio na fursa za baadaye;
   (c) Matokeo ya mradi (tathmini ya haja ya kufanya marekebisho ya mipango ya shughuli za mradi au matokeo tarajiwa, ikijumuisha hatua za kupunguza vihatarishi); na
   (d) Taarifa nyingine muhimu.

Matarajio

(a) Shughuli za mradi zilizopangwa kwa kipindi kinachofuata;
(b) Uendelevu (tathmini ya kiwango cha athari chanya za mradi); na
(c) Taarifa nyingine muhimu.

Dodoma,
21 Septemba, 2023

SELEMANI SAIDI JAFO,
*Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira*